**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

*Dar es Salaam*
*06 Februari, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA

## RAIS SAMIA AHITIMISHA ZIARA YA KIKAZI, UMOJA WA FALME ZA KIARABU (UAE)

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amehitimisha ziara yake ya kikazi Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), aliyoifanya kuanzia tarehe 02 Februari, 2026, kwa dhumuni la kushiriki Mkutano wa Serikali Duniani (WGS 2026) na kuendeleza diplomasia ya kiuchumi ya Tanzania.

Ziara hii ilikuwa ya kimkakati, ikilenga kuweka msingi wa ushirikiano wa muda mrefu baina ya Tanzania na nchi nyingine katika uwekezaji, biashara, na maendeleo, kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 na ajenda ya ajira kwa vijana.

Pembezoni mwa Mkutano huo, Rais Dkt. Samia alifanya mikutano ya ngazi ya juu na viongozi mbalimbali wa dunia, ikiwemo mazungumzo na Makamu wa Rais wa UAE na Mtawala wa Dubai, Mtukufu Sheikh Mohammed bin Rashid Al Maktoum, yaliyojikita katika kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi, uwekezaji, na ushiriki wa sekta binafsi katika ajenda ya maendeleo.

Aidha, alifanya mazungumzo na Waziri Mkuu wa Antigua na Barbuda, Mheshimiwa Gaston Browne, kuhusu kuimarisha ushirikiano kati ya Afrika na nchi za Karibiani kupitia Jumuiya ya Madola, hususan katika biashara na uwekezaji.

Rais Dkt. Samia pia alikutana na kuzungumza na Katibu Mkuu wa Shirika la Utalii la Umoja wa Mataifa *(UN Tourism),* Bi. Shaikha Al Nuwais, ambapo walijadili makubaliano ya pamoja ya kuimarisha sekta ya utalii na kuitangaza Tanzania kama kituo kikuu cha utalii endelevu duniani.

Halikadhalika, Rais Dkt. Samia alifanya mazungumzo ya kirafiki na viongozi mbalimbali, hatua iliyochangia kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia na kufungua fursa mpya za ushirikiano.

Vilevile, Rais Dkt. Samia alishiriki katika uzinduzi wa Jukwaa la Uwekezaji Afrika (GAIS), ambapo alisisitiza umuhimu wa mabadiliko ya sera za uwekezaji kutoka utegemezi wa misaada kwenda ushirikiano wa kibiashara unaochochea manufaa sawia ya rasilimali baina ya nchi na wawekezaji.

Halikadhalika, Rais Dkt. Samia aliwasilisha fursa za uwekezaji zilizopo Tanzania katika sekta za utalii, miundombinu, nishati, kilimo, viwanda, usafirishaji, na biashara ya kikanda, pamoja na kuainisha mageuzi yanayoendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini.

Ziara ya Rais Dkt. Samia nchini UAE imeweka msingi mzuri wa kuvutia uwekezaji wa baadaye na kuimarisha ushiriki wa wawekezaji wa ndani na wa kimataifa, unaoashiria mwanzo wa awamu mpya ya ushirikiano wa kiuchumi wa Tanzania na dunia, kwa lengo la kupata matokeo halisi katika uwekezaji, kuzalisha ajira, na ustawi wa wananchi.



Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu